Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | September-2026

EAJK

# Mikakati ya Ubishi katika Diskosi za Kisiasa za Nuru Okanga katika Bunge la Wananchi: Mtazamo wa Uchanganuzi Hakiki wa Diskosi

**Authors**
**Winnfred Ngina Wangai [(1)]; Harrison Ogutu Onyango [(2)]; Lina Akaka [(3)]**
**Main author's email: winnifredngina@gmail.com**

**(1.2) Catholic University of Eastern Africa, Kenya. (3) Kirinyaga University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Wangai, W. N., Onyango, H. O., & Akaka, L. (2026). Mikakati ya ubishi katika diskosi za kisiasa za Nuru Okanga katika Bunge la Wananchi: Mtazamo wa uchanganuzi hakiki wa diskosi. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 152–163. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1165

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-07-17
Accepted: 2026-08-08
Published: 2026-09-12

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya ubishi inayotumiwa na Nuru Okanga katika diskosi zake za kisiasa katika Bunge la Wananchi na kueleza kazi ya mikakati hiyo katika ujenzi na upinzani wa mamlaka. Ijapokuwa mijadala ya kisiasa nchini Kenya imezidi kujitokeza katika majukwaa yasiyo rasmi ya kiraia na kidijitali, tafiti nyingi za diskosi za kisiasa za Kiswahili zimejikita katika hotuba za viongozi wenye vyeo rasmi, wagombea wa uchaguzi, mijadala ya mabunge na diskosi zinazoripotiwa na vyombo vya habari. Utafiti uliongozwa na mhimili wa hegemonia na mabadiliko ya kijamii wa Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Diskosi ya Fairclough (2003). Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo wa kitaamuli katika Bunge la Wananchi, hususan Uwanja wa Jacaranda jijini Nairobi, huku YouTube ikitumika kama chanzo cha video za data. Kundi lengwa lilijumuisha video 24 za diskosi za kisiasa za Nuru Okanga zilizochapishwa kati ya 2024 na 2026, ambapo 12 ziliteuliwa kimakusudi. Data zilikusanywa kwa kutazama, kusikiliza na kunakili video hizo neno kwa neno, kisha kuchanganuliwa kwa hatua za kutambua, kueleza na kufasiri. Uchanganuzi ulibainisha mikakati mitano ya ubishi: kujisawiri vyema; kuwasawiri wapinzani vibaya na kuwabeza; uhalalishaji na uharamishaji wa mamlaka; kukata rufaa kwa hisia za hadhira; na ubandikaji majina pamoja na propaganda. Matokeo yanaonyesha kuwa mikakati hii huingiliana katika diskosi moja na hutumiwa kujenga taswira chanya ya msemaji, kudhoofisha uaminifu wa wapinzani, kuhoji uhalali wa mamlaka, kuamsha hisia za hadhira na kuunda utambulisho wa kisiasa. Utafiti unahitimisha kuwa lugha katika diskosi za Nuru Okanga hufanya kazi kama rasilimali ya kujenga mamlaka mbadala ya kijamii na kimaadili na kupinga mamlaka rasmi. Utafiti huu ni muhimu katika kupanua uelewa wa diskosi za kisiasa za Kiswahili katika majukwaa yasiyo rasmi na ya kidijitali.

**Maneno muhimu:** Bunge la Wananchi, diskosi za kisiasa, mamlaka, mikakati ya ubishi, uchanganuzi Hakiki wa diskosi, ushawishi.

**UTANGULIZI**

Utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya ubishi inayotumiwa na Nuru Okanga katika diskosi zake za kisiasa katika Bunge la Wananchi na kueleza kazi ya mikakati hiyo katika ujenzi na upinzani wa mamlaka. Diskosi ni matumizi ya lugha kama tendo la kijamii linaloweza kujenga, kudumisha na kupinga mahusiano ya mamlaka na itikadi katika jamii (Fairclough, 2003). Diskosi za kisiasa, kwa upande wake, huhusu matumizi ya lugha katika kujadili uongozi, utawala, sera, haki, uwajibikaji na masuala mengine ya maisha ya umma (Beard, 2000; Chilton, 2004). Kwa mtazamo huu, lugha ya kisiasa si chombo cha kuwasilisha taarifa pekee. Uteuzi wa maneno, namna msemaji anavyojitambulisha, namna anavyowasawiri wapinzani na namna anavyohusisha hadhira katika hoja vinaweza kutumika kujenga uhalali na kuathiri namna masuala ya kisiasa yanavyotafsiriwa.

Katika utafiti wa kisasa wa mawasiliano ya kisiasa, majukwaa ya kidijitali yameongeza njia ambazo wananchi wanaweza kufikia, kusambaza na kujadili diskosi za kisiasa. Kipkoech (2023), kwa kutumia data ya zaidi ya Wakenya 2,000, alichunguza uhusiano kati ya matumizi ya intaneti na habari za mitandao ya kijamii na ushiriki wa kisiasa nchini Kenya. Ingawa uhusiano chanya ulionekana katika uchanganuzi wa kimsingi, matokeo baada ya kudhibiti vigezo vingine hayakuonyesha uhusiano wa moja kwa moja wa kitakwimu. Jambo hili linaonyesha umuhimu wa kutenganisha madai kuhusu uwepo wa majukwaa ya kidijitali na madai kuhusu athari zake, na hivyo, utafiti huu haudai kuwa *YouTube* yenyewe ilisababisha ushiriki wa kisiasa.

Bunge la Wananchi ni muktadha muhimu wa kuchunguza aina hii ya diskosi. Lockwood (2019) anaonyesha kuwa Bunge la Wananchi limekuwa nafasi ya mjadala na uhamasishaji wa kisiasa wa kiwango cha chini, ambamo washiriki huunda lugha ya uraia, demokrasia na uwajibikaji. (Calleb Otieno et al., 2016) pia wanaonyesha kuwa harakati hiyo huunda nafasi za mijadala na uanaharakati katika anga ya umma ya mijini, huku mawasiliano yakisaidia kujenga mshikamano miongoni mwa washiriki. Utafiti wa Ohaga na Emojong (2024) unaonyesha zaidi kuwa Bunge la Mwananchi limekuwa jukwaa la kubadilishana taarifa na kuwasiliana kisiasa kwa muda mrefu, ingawa mijadala yake mara nyingi huingiliana na masimulizi yanayoibuka katika vyombo vya habari.

Uwanja wa Jacaranda nao ni muhimu kama muktadha wa uzalishaji wa diskosi. Hii ni kwa sababu, tafiti kuhusu Jacaranda Grounds zinaonyesha kuwa eneo hilo linaweza kutumika kama nafasi ya shughuli mbalimbali za kijamii na kisiasa, ikiwemo mikutano ya kisiasa na Bunge la Wananchi. Hivyo, katika utafiti huu, Jacaranda Grounds haichukuliwi kama sawa na YouTube. Bali, Jacaranda inachukuliwa kama mazingira halisi ambamo diskosi zilizalishwa na kutolewa ana kwa ana. Kwa upande mwingine, YouTube inachukuliwa kama chanzo cha video kilichotumiwa kufikia, kutazama tena na kunakili diskosi hizo.

Nuru Okanga ni mmoja wa wazungumzaji wanaojitokeza katika mijadala hii. Hii ni kwa sababu diskosi zake zinahusu masuala kama uongozi, uwajibikaji, gharama ya maisha, ukatili wa polisi, utambulisho wa kisiasa na mahusiano kati ya wananchi na viongozi. Kwa kuwa diskosi hizi hutolewa katika mazingira yasiyo rasmi na baadaye kusambazwa katika majukwaa ya kidijitali, zinatoa nafasi ya kuchunguza namna mzungumzaji asiye na wadhifa rasmi anavyotumia lugha kujenga uhalali, kuwasawiri wapinzani na kuhamasisha hadhira.

Pamoja na kuongezeka kwa tafiti kuhusu lugha ya kisiasa nchini Kenya, bado kuna pengo katika uchanganuzi wa mikakati ya ubishi ya mzungumzaji mmoja wa mashinani katika jukwaa lisilo rasmi. Kiplimo et al. (2026), kwa mfano, walichunguza deksia katika hotuba za Bunge la Mwananchi, lakini walijikita katika mshikamano wa matini. Muigai (2026) alichanganua sitiari za wanasiasa kama zilivyoripotiwa katika magazeti, huku data yake ikitokana na diskosi iliyoripotiwa na vyombo vya habari. Vivyo hivyo, Kiguta et al. (2024) walichunguza mikakati ya lugha katika diskosi ya ugaidi iliyowasilishwa katika magazeti. Tafiti hizi zinaonyesha utajiri wa lugha na ubishi katika diskosi za kisiasa, lakini hazichanganui kwa pamoja mikakati mitano inayolengwa na utafiti huu katika diskosi za moja kwa moja za Nuru Okanga.

Kwa msingi huo, utafiti huu ulilenga kubainisha mikakati ya ubishi inayotumiwa na Nuru Okanga katika diskosi zake za kisiasa katika Bunge la Wananchi na kueleza namna mikakati hiyo inavyohusiana na ujenzi

na upinzani wa mamlaka. Swali la utafiti lilikuwa: Ni mikakati ipi ya ubishi inayotumiwa na Nuru Okanga katika kujenga na kutetea hoja zake za kisiasa?

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Ubishi na Balagha katika Diskosi za Kisiasa

Beard (2000) ni kazi ya kinadharia inayochunguza lugha ya siasa na kuonyesha namna uteuzi wa lugha unavyoweza kujenga taswira ya mwanasiasa, kuwasawiri wapinzani na kuhalalisha misimamo. Chilton (2004), pia katika kazi ya kinadharia, anaeleza namna diskosi za kisiasa zinavyohusisha ujenzi wa "sisi" na "wao", uhalalishaji wa hatua na udhibiti wa mitazamo ya hadhira. Charteris-Black (2005) anaunganisha uchanganuzi wa diskosi na balagha, akionyesha namna sitiari zinavyoweza kubeba tathmini ya kisiasa na kujenga ushawishi. Kazi hizi hazipaswi kuchukuliwa kama tafiti za kiempiriki zinazofanana na data ya makala hii; mchango wao hapa ni kutoa dhana na misamiati ya uchanganuzi.

Khajavi na Rasti (2020) walifanya utafiti wa kiempiriki wa hotuba 30 za kampeni ya urais wa Marekani mwaka 2012, wakichanganua mikakati ya balagha na ushawishi. Walibaini, miongoni mwa mikakati mingine, kujisawiri vyema, kuwasawiri wapinzani vibaya, uhalalishaji na uharamishaji. Utafiti huu una uhusiano wa moja kwa moja na utafiti huu kwa sababu unatumia kazi ya kihoja kama msingi wa uainishaji. Tofauti muhimu ni kwamba data ya Khajavi na Rasti ilitokana na wagombea rasmi wa urais, wakati utafiti huu unahusu mzungumzaji asiye na wadhifa rasmi katika jukwaa la kiraia. Kamuru et al. (2025) walichunguza balagha katika hotuba za William Ruto na Raila Odinga katika makongamano ya wajumbe nchini Kenya. Utafiti wao, ulioongozwa na Nadharia ya Balagha ya Aristotle, ulibaini matumizi ya mantiki, kigusahisi na maadili katika kujenga imani, kugusa hisia na kuonyesha uwezo wa uongozi. Matokeo haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa yanaonyesha nafasi ya hisia na ujenzi wa uaminifu katika mawasiliano ya kisiasa ya Kenya. Hata hivyo, utafiti wao ulijikita katika wagombea wawili wa urais, si mzungumzaji wa jukwaa lisilo rasmi.

### Diskosi za Kisiasa, Bunge la Wananchi na Muktadha wa Kenya

Habwe (1999) aliweka msingi muhimu wa kuchunguza diskosi za kisiasa za Kiswahili nchini Kenya. Hata hivyo, data hiyo ilikusanywa kabla ya mabadiliko makubwa ya mazingira ya kidijitali na kabla ya kuenea kwa majukwaa kama *YouTube* na mitandao ya kijamii katika mawasiliano ya kisiasa. Kwa hiyo, kazi yake inatumika hapa kama msingi wa kihistoria wa usomi wa diskosi za Kiswahili, si kama ushahidi wa kutosha wa mazingira ya sasa. Kimari na Rasmussen (2010) walichunguza nafasi za umma na siasa zisizo rasmi jijini Nairobi, wakionyesha namna nafasi za umma zinavyoweza kuwa maeneo ya mazungumzo na ushiriki wa kisiasa. Lockwood (2019) alipanua mjadala huu kwa kuchunguza Bunge la Wananchi na kuonyesha namna lugha ya uraia, demokrasia na uwajibikaji inavyotumiwa katika uhamasishaji wa kisiasa. (Calleb Otieno et al., 2016), walisisitiza pia umuhimu wa mawasiliano katika kujenga mshikamano wa harakati za Bunge la Mwananchi.

Vivo hivyo, Ohaga na Emojong (2024) walichunguza mijadala ya Bunge la Mwananchi kwa kutumia Nadharia ya Uwanja wa Umma. Walibaini kuwa Bunge la Mwananchi limekuwa jukwaa la kubadilishana taarifa linalotumiwa na wanasiasa, wanaharakati na wananchi wa kawaida. Kiplimo et al. (2026) walichunguza hotuba za Bunge la Mwananchi katika Jacaranda na kubaini kuwa deksia huchangia mshikamano wa matini. Tafiti hizi ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu zinathibitisha kuwa Bunge la Mwananchi na Jacaranda ni mazingira yanayofaa kuchunguza mawasiliano ya kisiasa, lakini malengo yao hayakuwa uchanganuzi wa mikakati ya ubishi ya mzungumzaji mmoja.

Katika upande wa mawasiliano ya kidijitali, Kipkoech (2023) alichunguza uhusiano kati ya matumizi ya habari za mtandao na ushiriki wa kisiasa nchini Kenya. Kariuki na Gichanga (2025) walichunguza uratibu wa mitandao ya kijamii katika uhamasishaji wa kisiasa wa Kenya mwaka 2024 na kuonyesha namna mawasiliano ya kidijitali yalivyowezesha uhamasishaji unaopita mipaka ya miundo ya kawaida ya kisiasa. Kazi hizi zinaonyesha umuhimu wa kuzingatia uhusiano kati ya diskosi za ana kwa ana na usambazaji wa kidijitali, bila kudai kwamba jukwaa la kidijitali lenyewe ndilo chanzo cha athari za kisiasa.

**Mikakati ya Uhalalishaji, Uharamishaji na Uwasawiri wa Wapinzani**

Dimbu et al. (2025) walichunguza mkakati wa uhalalishaji wa kimamlaka katika hotuba teule za marais wa Tanzania katika vikao vya pamoja vya mabunge ya kitaifa nchini Kenya. Utafiti wao unaonyesha namna viongozi wenye mamlaka rasmi wanavyotumia lugha kujenga uhalali wa mamlaka. Utafiti huu unahamisha swali hilo kwenda kwa mzungumzaji asiye na mamlaka ya kikatiba, na hivyo kuuliza namna uhalali unavyoweza kudaiwa kutoka nje ya taasisi rasmi.

Vilevile, Kiguta et al. (2024) walitumia nadharia ya ubishi kuchanganua diskosi ya ugaidi katika magazeti ya Kenya na ya kimataifa. Walibaini matumizi ya mikakati ya lugha na itikadi katika kuunda mitazamo kuhusu makundi yanayokinzana. Muigai (2026) naye alibaini kuwa sitiari katika usemi wa wanasiasa wa Kenya zinaweza kutumika kuwashambulia na kuwaondolea uhalali wapinzani. Tafiti hizi zinaunga mkono umuhimu wa kuchunguza uwasawiri hasi, lebo na sitiari kama sehemu ya kazi pana ya kihoja.

**Pengo la Utafiti**

Kwa jumla, maandiko yaliyopitiwa yanaonyesha misingi mitatu. Kwanza, kazi za kinadharia zinaonyesha kuwa lugha ya kisiasa ni sehemu ya ujenzi wa mamlaka, utambulisho na ushawishi. Pili, tafiti za kiempiriki za Kenya na Afrika Mashariki zinaonyesha matumizi ya balagha, uhalalishaji, sitiari na mikakati ya ubishi katika diskosi za kisiasa. Tatu, tafiti za Bunge la Mwananchi na mawasiliano ya kidijitali zinaonyesha umuhimu wa majukwaa yasiyo rasmi na ya kidijitali katika maisha ya kisiasa. Hata hivyo, bado kuna pengo katika kuchanganua kwa pamoja mikakati ya kujisawiri, uwasawiri hasi wa wapinzani, uhalalishaji/uharamishaji, rufaa ya hisia na ubandikaji majina/propaganda katika diskosi za mzungumzaji mmoja wa mashinani. Hilo ndilo pengo linaloshughulikiwa na makala hii.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Diskosi ya Fairclough (2003), kwa msisitizo katika dhana ya hegemonia na mabadiliko ya kijamii. Kwa mtazamo wa Fairclough, diskosi huunganishwa na mahusiano ya kijamii na kimamlaka na inaweza kuwa sehemu ya kudumisha au kupinga mpangilio uliopo. Hegemonia husaidia kueleza jinsi mitazamo fulani inavyoweza kuwasilishwa kama ya kawaida na halali, na jinsi diskosi mbadala zinavyoweza kuhoji hali hiyo. Katika makala hii, nadharia iligeuzwa kuwa utaratibu wa uchanganuzi kwa hatua tatu. Kwanza, kutambua sehemu ambazo msemaji anajenga uhalali wa nafsi yake au anawapa wengine sifa fulani. Pili, kueleza kazi ya kiisimu na kihoja ya sehemu hiyo, kwa mfano kujisawiri, kudhoofisha mpinzani au kuamsha hisia. Tatu, kufasiri namna kazi hiyo inavyohusiana na mahusiano ya mamlaka, itikadi na upinzani wa hegemonia.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo wa kitaamuli. Muundo huu ulifaa pale ambapo mtafiti alilenga kueleza na kufasiri maana, matumizi na kazi za lugha katika mazingira yake halisi badala ya kupima uhusiano wa kitakwimu kati ya vigezo (Creswell, 2014; Kothari, 2004). Kwa kuwa lengo la utafiti huu lilikuwa kuchanganua kazi za kihoja katika matini za diskosi, muundo huu uliwezesha mtafiti kuhifadhi muktadha wa matamshi na kuhusisha lugha na mahusiano ya kijamii na kimamlaka.

Eneo la utafiti lilikuwa Bunge la Wananchi, hususan Uwanja wa Jacaranda jijini Nairobi. Hii ni kwa sababu hapa ndipo diskosi zilizotafitiwa zilitolewa ana kwa ana. *YouTube* haikuchukuliwa kuwa eneo la utafiti, bali chanzo cha data ya video. Video zilizotolewa Jacaranda zilipatikana kupitia *YouTube*, ambako ziliweza kutazamwa mara kadhaa, kusikilizwa na kunakiliwa. Tofauti hii ni muhimu kwa sababu muktadha wa uzalishaji wa diskosi ni Jacaranda, wakati jukwaa la kidijitali ni njia ya kufikia kumbukumbu ya tukio.

Kundi lengwa lilijumuisha video 24 za diskosi za Nuru Okanga zilizopatikana *YouTube* na kuchapishwa kati ya 2024 na 2026. Video 12 ziliteuliwa kimakusudi. Vigezo vya ujumuishaji vilikuwa: Nuru Okanga kuwa mzungumzaji mkuu; video kuhusishwa na Bunge la Wananchi; kuchapishwa katika kipindi kilicholengwa; kuwa na sauti na picha zinazowezesha unukuzi; na kuwa na maudhui yanayohusiana na lengo la utafiti. Video zilizokuwa nakala za video nyingine, zisizokuwa na diskosi ya kutosha au zenye ubora usioruhusu unukuzi sahihi zilitengwa.

Kwa kuongeza, data zilikusanywa kwa kutazama na kusikiliza kila video mara kadhaa na kunakili dondoo husika neno kwa neno. Uhamishaji msimbo, mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza na vipengele vya lugha ya mazungumzo vilihifadhiwa pale vilipojitokeza kwa sababu vilikuwa sehemu ya matini yenyewe. Kila video iliwekewa msimbo D1 hadi D12. Data ilichanganuliwa kimaelezo kwa hatua za kutambua, kueleza na kufasiri.

Kwa upande wa maadili, data zilitokana na video zilizowekwa hadharani. Matumizi yake yalilenga uchanganuzi wa kitaaluma, na dondoo ziliwasilishwa kama matamshi ya mzungumzaji katika muktadha wa utafiti. Madai ya kisiasa yaliyomo katika dondoo hayakuchukuliwa kama ukweli wa nje ya matini bila uthibitisho huru.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Uchanganuzi wa video 12 ulibainisha mikakati mitano ya ubishi. Ili kujibu hoja ya ukosefu wa mshikamano wa viwango vya uchanganuzi, mikakati yote mitano imeainishwa kwa kigezo kimoja: kazi kuu ya kihoja. Kwa hiyo, "kuwasawiri wapinzani vibaya na kuwabeza" inachukuliwa kama kundi moja kwa sababu vipengele vyake vina kazi kuu ya kudhoofisha uaminifu na hadhi ya mpinzani. Vivyo hivyo, "ubandikaji majina na propaganda" inachukuliwa kama kundi moja kwa sababu lebo zinazobandikwa kwa watu au makundi hutumiwa kama sehemu ya ujenzi wa masimulizi ya kisiasa yenye hukumu iliyorahisishwa. Majina haya yanaeleza kazi ya mkakati, si aina moja ya kifaa cha lugha.

**Jedwali 1: Mikakati ya Ubishi Iliyobainishwa**

| Mkakati | Kazi kuu ya kihoja | Mifano ya data |
|---|---|---|
| Kujisawiri vyema | Kujenga taswira chanya ya msemaji na uaminifu wake | D1, D9, D12 |
| Kuwasawiri wapinzani vibaya na kuwabeza | Kudhoofisha uaminifu, hadhi au sifa ya mpinzani | D1, D5, D7, D9 |
| Uhalalishaji na uharamishaji wa mamlaka | Kujenga uhalali wa msimamo na kuhoji uhalali wa mamlaka pinzani | D1, D3, D5, D6 |
| Kukata rufaa kwa hisia za hadhira | Kuamsha huruma, hofu, hasira, mapenzi au mshikamano | D1, D2, D5 |
| Ubandikaji majina na propaganda | Kuunda lebo na masimulizi yanayorahisisha hukumu ya kisiasa | D4, D6, D12 |

**Kujisawiri Vyema**

Kujisawiri vyema ni mkakati wa kujenga taswira chanya ya msemaji ili kuimarisha uaminifu wa hadhira kwake. Katika data hii, mkakati huo hujengwa kupitia madai ya uanzilishi, uwezo wa kiakili, uwajibikaji na ukaribu na wananchi.

*"Mimi kama Nuru Okanga ndio nilianza kuongea kwa social media ndio hao watu wengine wengine wakafanya nini."* (Dondoo: D1).

Dondoo hili linajenga taswira ya msemaji kama mwasisi. Neno "nilianza" linaweka historia ya msemaji mbele ya historia ya wengine na kumwezesha kudai hadhi ya uongozi wa kimawazo. Kazi kuu ya kihoja hapa ni kujenga uaminifu kwa kutumia historia ya kibinafsi, si kutoa taarifa ya kisiasa pekee.

Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), dai la uanzilishi linaweza kusomwa kama jaribio la kuunda chanzo cha uhalali nje ya taasisi rasmi. Msemaji hana wadhifa wa kikatiba, kwa hiyo historia anayojiwekea katika diskosi inakuwa rasilimali ya kujenga mamlaka mbadala. Hoja hii inalingana na Khajavi na Rasti (2020), ambao walionyesha umuhimu wa kujisawiri chanya katika kujenga uaminifu wa awali, ingawa data yao ilihusu wagombea rasmi.

*"Mtu mwenye hajasoma anaweza jua majina ya hao watu wote? I'm very clever man! Mimi naweza kutajia the whole magavana account 47 lakini wewe huwezi."* (Dondoo: D9).

Hapa, msemaji anabadilisha ukosefu wa elimu rasmi kuwa hoja ya uwezo wa kiakili. Swali la balagha linatengeneza changamoto kwa dhana kwamba elimu

rasmi ndiyo kipimo pekee cha uwezo. Kauli "I'm very clever man!" kisha inatoa jibu la moja kwa moja kuhusu taswira anayojenga. Kazi ya mkakati ni kuhalalisha usikivu kwake kwa kutumia maarifa ya vitendo.

Kwa Fairclough (2003), diskosi hii inahoji kipimo cha kijamii cha thamani kinachotegemea elimu rasmi. Hata hivyo, uchanganuzi huu hauhakikishi kwamba msemaji ana uwezo huo kwa maana ya kielimu; unaeleza namna anavyojenga taswira hiyo ndani ya matini. Hivyo, mkakati huu unaonyesha uhusiano kati ya kujisawiri na mapambano ya kijamii kuhusu nani anastahili kusikilizwa katika siasa.

*"Hiyo ndio namba yangu, sijawahi badilika, sijawahi badilisha, na hiyo namba hata nikiwa MCA itakuwa on throughout."* (Dondoo: D12).

Dondoo hili linajenga taswira ya uwazi na upatikanaji. Ahadi ya kutobadilisha namba ya simu hata baada ya kupata wadhifa inalenga kuonyesha kwamba msemaji hatabadilika baada ya kupata mamlaka. Kazi kuu ya kihoja ni kuwasilisha uaminifu wa baadaye kabla ya mamlaka hiyo kupatikana. Kwa hiyo, kujisawiri vyema katika data hakutegemei kujisifu pekee. Kunahusisha pia kujenga uhusiano wa karibu na wananchi, kuonyesha uwezo wa vitendo na kuahidi mwendelezo wa uhusiano huo. Hali hii inapanua mjadala wa Khajavi na Rasti (2020) kwa kuonyesha namna mkakati huo unavyoweza kufanya kazi kwa mzungumzaji asiye na wadhifa rasmi.

**Kuwasawiri Wapinzani Vibaya na Kuwabeza**

Kundi hili linahusu matumizi ya lugha yenye kazi kuu ya kupunguza uaminifu, hadhi au sifa ya mpinzani. Vipengele kama dharau, lebo za udhaifu, sitiari za hatari na tuhuma za kifedha vinawekwa pamoja kwa sababu vinafanya kazi moja ya kihoja: kuunda taswira hasi ya upande pinzani.

*"Inafaa mjue Ruto ni sumu."* (Dondoo: D7).

Neno "sumu" linamjenga Rais Ruto kama chanzo cha madhara, badala ya kiongozi anayepingwa kwa sera au hatua maalumu. Sitiari hii ni fupi, lakini inabeba hukumu pana. Kazi yake ya kihoja ni kudhoofisha uaminifu wa mhusika kwa kumhusisha na hatari. Kwa mujibu wa Charteris-Black (2005), sitiari za kisiasa huweza kubeba tathmini ya kisiasa ndani ya taswira moja. Muigai (2026) pia alibaini kuwa sitiari katika diskosi za wanasiasa wa Kenya zinaweza kutumiwa kuwashambulia na kuwaondolea uhalali wapinzani. Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), uchaguzi wa sitiari hii unaingia katika mapambano ya kimamlaka kwa sababu unabadilisha tathmini ya kiongozi kutoka mjadala wa sera kwenda hukumu kuhusu tabia na madhara yake.

*"Mimi tangu nizaliwe sijawahi ona mwanaume mjinga kama Opiyo Wandayi."* (Dondoo: D1).

Kauli hii inatumia dharau ya moja kwa moja pamoja na chuku. Kirai "tangu nizaliwe" kinapanua hukumu kutoka tukio au sera maalumu hadi uzoefu wote wa maisha wa msemaji. Kazi yake ni kuifanya lebo "mjinga" ionekane kuwa hukumu iliyothibitishwa na uzoefu wa muda mrefu wa msemaji.

Hapa, dharau inafanya kazi pamoja na kujisawiri. Msemaji anapomweka mpinzani katika nafasi ya kutokuwa na akili, anajenga kwa njia isiyo ya moja kwa moja taswira yake mwenyewe kama mwenye uelewa zaidi. Hali hii inaendana na ujenzi wa "sisi" na "wao" unaoelezwa katika diskosi za kisiasa (Chilton, 2004; van Dijk, 1998).

*"Junet ndiye alikula pesa ya Raila Odinga mpaka baba akaanguka kura."* (Dondoo: D5).

Dondoo hili linatumia tuhuma ya kifedha kumhusisha mhusika mmoja na matokeo ya kisiasa. Neno "alikula pesa" linabeba maana ya matumizi mabaya ya fedha, huku kushindwa kwa kampeni kukihusishwa na mhusika mmoja. Kazi kuu ya kihoja ni kumhamishia mpinzani lawama na, kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kumtenga msemaji na chanzo cha lawama.

Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), tuhuma kama hii inapaswa kueleweka kama sehemu ya mapambano ya ndani kuhusu uongozi na uwajibikaji. Utafiti huu haithibitishi tuhuma hiyo kama ukweli wa nje; inachanganua namna tuhuma hiyo inavyotumika katika diskosi. Hivyo, ushahidi wa data unaonyesha kazi ya lugha, si uthibitisho wa madai ya kisiasa.

Kwa jumla, mkakati huu unaonyesha kwamba usawiri hasi unaweza kulenga adui wa kitaifa, mshirika wa

kisiasa au mtu anayehusishwa na migogoro ya ndani. Kigezo cha kuwaweka katika kundi moja ni kazi ya kihoja, si aina ya lugha iliyotumiwa.

**Uhalalishaji na Uharamishaji wa Mamlaka**

Mkakati huu unahusu kujenga uhalali wa msimamo wa msemaji na wakati huo huo kuhoji au kudhoofisha uhalali wa mamlaka pinzani. Uhalalishaji na uharamishaji vinaweza kutokea katika dondoo moja, kwa sababu kuuharamisha upande mmoja kunaweza kuimarisha upande mwingine (van Dijk, 1998).

*"Mimi sikukuchagua, ilipigia Raila Odinga kwa bahati mbaya ukaimba ukatoboa, uliibia Raila Odinga na ukatoboa wewe ndio president."* (Dondoo: D3).

Msemaji anahoji chanzo cha uhalali wa urais wa Ruto kwa kuwasilisha uchaguzi kama usioakisi matakwa ya wapiga kura aliowawakilisha. Kazi ya mkakati hapa ni kuhamisha mjadala kutoka hadhi rasmi ya Rais kwenda kwenye swali la uhalali wa jinsi mamlaka hiyo ilivyopatikana.

Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), diskosi hii inahusisha mapambano kuhusu maana ya mamlaka halali. Msemaji anapinga uhalali wa taasisi au mchakato wa kisiasa kwa kutumia simulizi la uchaguzi. Dimbu et al. (2025) walionyesha upande mwingine wa mchakato huu, ambapo viongozi wenye mamlaka rasmi hutumia lugha kujenga uhalali wa mamlaka. Tofauti hii inaonyesha kuwa uhalalishaji si rasilimali ya walio madarakani pekee; pia inaweza kudaiwa na wapinzani wao.

*"Ulipeleka Raila Odinga Bondo but spirit ya Raila Odinga iko Jakaranda. Mimi ni spirit ya Raila Odinga niko hapa."* (Dondoo: D1).

Dondoo hili linajenga uhalali wa msemaji kwa kujihusisha na urithi wa kisiasa wa Raila Odinga. Kirai "spirit ya Raila Odinga" kinamweka msemaji katika nafasi ya mwendelezaji wa urithi wa kisiasa na hivyo kujenga mamlaka ya kiishara. Kazi ya kihoja si kuthibitisha urithi huo kwa njia ya kitaasisi, bali kuunda uhalali unaotegemea uhusiano wa kiishara na hisia za hadhira.

Kulingana na Fairclough (2003), huu ni mfano wa diskosi inayojenga chanzo mbadala cha uhalali. Msemaji anatumia kumbukumbu na urithi wa kisiasa kama rasilimali ya mamlaka. Hapa uhalalishaji unaingiliana na rufaa ya hisia, jambo linaloonyesha kwa nini mikakati ya ubishi haiwezi kuchukuliwa kama visanduku vinavyotenganishwa kabisa.

*"Kama Ruto unafanya kazi fair and free, toka nje upeane list yote ya maparastatal wale wanaongoza ni kabila gani."* (Dondoo: D5).

Muundo wa "kama... toka nje..." unaweka sharti ambalo mwenye mamlaka anatakiwa kulijibu. Msemaji hatangazi tu kwamba mfumo wa uteuzi si wa haki; anadai uwazi kama kipimo cha haki. Kwa hiyo, dondoo hili ni mfano wa uharamishaji wa masharti: uhalali wa mchakato unawekwa chini ya jaribio la uwazi.

Mhimili wa hegemonia wa Fairclough (2003) unasaidia kueleza kwa nini uwazi unakuwa eneo la mapambano ya kimamlaka. Mamlaka rasmi hujaribu kuwasilisha utaratibu wake kama wa kawaida na halali, huku msemaji akiulazimisha mfumo huo kujieleza kwa hadhira.

*"Ruto mwenyewe ako kwa uongozi kwa sababu ya katiba. Tutaheshimu watu wa upinzani, heshimu watu wa upinzani, Mr William Samoei Ruto."* (Dondoo: D6).

Dondoo hili linaonyesha uhalalishaji wa masharti. Msemaji anakubali chanzo cha kikatiba cha mamlaka ya Ruto, lakini anadai kwamba mamlaka hayo yatumiwe kwa kuheshimu wapinzani. Hivyo, mkakati haupingi mfumo mzima wa kikatiba. Unatumia uhalali wa mfumo huo kama msingi wa kumdai mwenye mamlaka awajibike kwa kanuni za usawa.

Mifano hii inaonyesha kuwa uhalalishaji na uharamishaji si kinyume rahisi cha "kuunga mkono" dhidi ya "kupinga". Katika diskosi moja, msemaji anaweza kuharamisha chanzo cha mamlaka, kudai uhalali wa urithi wake mwenyewe na wakati mwingine kukubali uhalali wa kikatiba wa mpinzani huku akihoji namna mamlaka hayo yanavyotumiwa.

**Kukata Rufaa kwa Hisia za Hadhira**

Mkakati huu unahusu matumizi ya lugha yanayolenga kuamsha huruma, hofu, hasira, mapenzi, mshikamano au hisia nyingine za hadhira. Kamuru et al. (2025) walionyesha kuwa kigusahisi ni mhimili muhimu wa

balagha ya kisiasa nchini Kenya. Katika data hii, rufaa ya hisia hutokana na takwimu, taswira ya mgogoro, uhusiano wa kifamilia na simulizi za uzoefu wa wananchi.

*"Hawa wananchi wale wamesimama hapa zaidi ya vichwa 3000... kati ya 3,000, 500 ndio wameweka chakula kwa meza, 2500 hawajaweka."* (Dondoo: D1).

Dondoo hili linatumia idadi kubwa ya watu kugeuza suala la chakula kuwa tatizo la pamoja. Msemaji anachagua takwimu ya watu 3,000 na kisha kutenganisha wale wanaodaiwa kuwa na chakula na wale wasiokuwa nacho. Kazi ya kihoja ni kuamsha huruma na kufanya suala la gharama ya maisha lionekane kama uzoefu wa watu halisi.

Kulingana na Fairclough (2003), matumizi haya yanaunganisha matini na hali ya kijamii inayodaiwa na msemaji. Hata hivyo, kwa kuwa utafiti huu haukufanya uhakiki huru wa takwimu hiyo, uchanganuzi unaangazia kazi yake ya kidiskosi, si ukweli wa kitakwimu wa dai hilo.

*"Tuko vibaya Mr Speaker, tuko vibaya na tuko vibaya na tuko vibaya na tuko vibaya na Kenya yuko ICU."* (Dondoo: D2).

Takriri ya "tuko vibaya" hujenga mfululizo wa hisia unaofikia kilele katika "Kenya yuko ICU." Taifa linawasilishwa kama mgonjwa aliye katika hali ya dharura. Kazi ya kihoja ni kuifanya hali ya kisiasa na kiuchumi ionekane ya haraka na yenye hatari, na hivyo kuimarisha hitaji la hatua. Matokeo haya yanaendana na Kamuru et al. (2025), ambao walibaini kuwa kigusahisi hutumiwa katika diskosi za kisiasa kujenga hisia na ushawishi. Tofauti ni kwamba hapa rufaa ya hisia inatokea katika jukwaa lisilo rasmi na inahusisha lugha ya mazungumzo, takriri na sitiari kwa pamoja.

*"Nataka niambie polisi nyinyi ni mandugu zetu, ile uchumi tunapitia sijui nyinyi mnanunua wapi unga na sisi tunanunua wapi."* (Dondoo: D5).

Dondoo hili linatumia lugha ya undugu kujaribu kupunguza mpaka kati ya wananchi na polisi. Msemaji anaanza kwa kuwaita polisi "mandugu zetu" kisha anawaunganisha na uzoefu wa gharama ya maisha. Kazi ya mkakati ni kujenga mshikamano badala ya uhasama na kuonyesha kuwa makundi hayo mawili yanakabiliwa na hali ya kiuchumi inayofanana.

Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), hii ni muhimu kwa sababu rufaa ya hisia inaweza kutumiwa si tu kumshambulia mpinzani, bali pia kumshawishi mhusika anayechukuliwa kuwa sehemu ya mfumo wa mamlaka. Hivyo, hisia inakuwa rasilimali ya kujenga muungano wa kijamii.

*"Babu na babu kwa sababu bila babu ni taabu."* (Dondoo: D5)

Lakabu "Babu" linamjenga Raila Odinga kama mhusika wa kifamilia na hivyo kuimarisha ukaribu wa kihisia. Mnyambuliko wa "babu" na "taabu" pia huifanya kauli iwe rahisi kukumbuka. Hapa hisia ya mapenzi na heshima ya kifamilia inatumika kujenga mshikamano wa kisiasa.

Kwa jumla, rufaa ya hisia katika data haitegemei aina moja ya hisia. Inabadilika kutoka huruma ya kiuchumi, hofu ya kitaifa, mshikamano na polisi hadi mapenzi ya kifamilia. Utofauti huu unaonyesha uwezo wa mkakati huo kubadilika kulingana na hadhira na lengo la hoja.

**Ubandikaji Majina na Mikakati ya Kipropaganda**

Mkakati huu unahusu matumizi ya lebo fupi zinazoweka watu, makundi au mifumo katika taswira chanya au hasi. Ubandikaji majina na propaganda umewekwa katika kundi moja kwa sababu kazi yake kuu katika data ni kurahisisha hukumu ya kisiasa na kuunda mipaka ya utambulisho. Hivyo, si kila lebo ni propaganda kwa maana pana, bali lebo zinachanganuliwa kama sehemu ya ujenzi wa masimulizi ya kisiasa.

*"Kuna mabwenyenye wanaiba mali yetu, wanakula mzuri zuri, wanakula pesa yetu Mr Spika na wakenya wanalia."* (Dondoo: D4).

Neno "mabwenyenye" linaunda kundi la "wao" linalowekwa dhidi ya "wakenya". Badala ya kutaja watu mmoja mmoja, msemaji anatumia lebo ya kitabaka kuwakusanya watu anaowaona kuwa wanatumia rasilimali za umma vibaya. Kazi ya kihoja ni kurahisisha mgawanyiko wa kisiasa kuwa kati ya kundi linalodaiwa kunufaika na kundi linalodaiwa kuumia.

Kwa Fairclough (2003), lebo kama hii inaweza kuonyesha na wakati mwingine kuimarisha mgawanyiko wa kitabaka katika diskosi. Hata hivyo,

uchanganuzi hauchukui madai ya wizi kama ukweli uliothibitishwa; unachanganua namna lebo hiyo inavyotumika kujenga taswira ya mpinzani.

*"Hata pia mimi ni mdozu wa Ruto, natoa taksi... Lazima aheshimu wadozi wake. Wakenya ni wadozi wa Ruto."* (Dondoo: D6).

Neno "wadozi" linabadilisha uhusiano kati ya wananchi na serikali kuwa uhusiano wa kimkataba. Wananchi wanawasilishwa kama watu wanaochangia kwa kodi, huku serikali ikiwekwa katika nafasi ya mpokeaji anayepaswa kuheshimu waliotoa rasilimali. Kazi ya lebo hii ni kujenga utambulisho wa pamoja wa wananchi na kuhalalisha madai yao ya uwajibikaji. Hapa, propaganda haijitokezi kama uongo wa moja kwa moja, bali kama ujenzi wa fremu ya kutafsiri uhusiano wa kisiasa. Msemaji anachagua neno linaloweza kuwafanya wananchi wajione kama kundi lenye haki ya kudai heshima. Hivyo, lebo inaweza kujenga mshikamano chanya wa "sisi" badala ya kumshambulia mtu mmoja.

*"Ati affordable house, ati Ruto anajenga manyumba. Wakenya nawaambianga kila siku mimi sijasoma lakini niko na akili, sio Ruto anajenga manyumba ni Wakenya wanajijengea manyumba."* (Dondoo: D12).

Kurudiwa kwa "ati" kunatia shaka katika kauli rasmi kuhusu mradi wa nyumba nafuu. Kisha msemaji anabadilisha fremu ya mradi kutoka "Ruto anajenga" kwenda "Wakenya wanajijengea". Hivyo, kazi ya kihoja ni kuhamisha sifa ya sera kutoka kwa serikali kwenda kwa wananchi na kuunda simulizi mbadala kuhusu nani anayebeba gharama na nani anayepaswa kupata sifa.

Vilevile, Muigai (2026) alibaini kuwa lugha ya kisitiari na ujenzi wa mipaka ya kisiasa vinaweza kutumika kuunda makundi ya ndani na nje. Mifano hii inaonyesha kuwa ubandikaji majina unaweza kuwa wa hasi, kama "mabwenyenye", au wa kujenga utambulisho wa pamoja, kama "wadozi". Kigezo cha kundi hili ni kazi ya lebo katika kupanga tafsiri ya kisiasa, si thamani yake ya kimaadili.

**Muhtasari wa Matokeo**

**Jedwali 2: Uhusiano wa Mikakati ya Ubishi na Kazi Zake**

| Mkakati | Kazi ya msingi | Mamlaka/uhusiano unaojengwa |
|---|---|---|
| Kujisawiri vyema | Kujenga uaminifu na taswira chanya | Mamlaka ya kimawazo, kimaadili na ya uzoefu |
| Kuwasawiri wapinzani vibaya na kuwabeza | Kudhoofisha hadhi na uaminifu wa wapinzani | Mipaka ya "sisi" na "wao" |
| Uhalalishaji na uharamishaji wa mamlaka | Kujenga uhalali na kuhoji uhalali wa wengine | Mamlaka mbadala dhidi ya mamlaka pinzani |
| Kukata rufaa kwa hisia za hadhira | Kuamsha huruma, hofu, hasira na mshikamano | Muungano wa kihisia kati ya msemaji na hadhira |
| Ubandikaji majina na propaganda | Kuunda lebo na fremu za kutafsiri siasa | Utambulisho wa makundi na masimulizi mbadala |

Matokeo yanaonyesha kuwa mikakati mitano haifanyi kazi kama vitengo vilivyotengwa. Dondoo moja linaweza kutekeleza zaidi ya kazi moja. Kwa mfano, kauli kuhusu "spirit ya Raila Odinga" inajenga taswira ya msemaji, inadai uhalali wa kiishara na wakati huo huo inakata rufaa kwa hisia za wafuasi wa Raila Odinga. Hata hivyo, uainishaji wa mikakati umefanywa kwa kuzingatia kazi kuu ya kihoja ili kuzuia kuchanganya viwango tofauti vya uchanganuzi.

Kwa mtazamo wa Fairclough (2003), mwingiliano huu unaonyesha kwamba diskosi ni sehemu ya mapambano ya kijamii kuhusu mamlaka na maana. Msemaji asiye na wadhifa rasmi anatumia historia yake, uhusiano wa kiishara, lugha ya undugu, lebo za makundi na masimulizi ya wananchi kujenga uhalali wa kijamii. Wakati huo huo, anatumia uharamishaji, usawiri hasi na maswali ya changamoto kuhoji mamlaka pinzani. Hivyo, hegemonia haionekani kama mfumo uliokamilika usiopingika; inaonekana kama eneo la mapambano la maana na uhalali.

Matokeo haya yanaendana na Khajavi na Rasti (2020) katika kutambua kujisawiri, uwasawiri hasi na uhalalishaji/uharamishaji kama mikakati muhimu ya diskosi za kisiasa. Yanaendana pia na Kamuru et al. (2025) kuhusu nafasi ya hisia katika ushawishi wa kisiasa na Dimbu et al. (2025) kuhusu uhalalishaji wa mamlaka. Hata hivyo, mchango wa utafiti huu ni kuonyesha namna mikakati hiyo inavyofanya kazi katika diskosi ya mzungumzaji wa mashinani asiye na wadhifa rasmi na katika mazingira yanayounganisha jukwaa la ana kwa ana na usambazaji wa kidijitali.

Ni muhimu pia kutofautisha kazi ya kihoja na athari halisi kwa hadhira. Kwa kuwa utafiti huu haukukusanya data kutoka kwa wasikilizaji, hauwezi kuthibitisha kwamba hadhira ilishawishika, iliamini madai ya msemaji au ilibadilisha tabia kwa sababu ya mikakati hiyo. Utafiti unaonyesha kazi za kihoja zinazoweza kutambuliwa ndani ya matini. Utafiti wa mapokezi ungehitajika kuthibitisha athari hizo.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Utafiti huu ulibainisha mikakati mitano: kujisawiri vyema; kuwasawiri wapinzani vibaya na kuwabeza; uhalalishaji na uharamishaji wa mamlaka; kukata rufaa kwa hisia za hadhira; na ubandikaji majina pamoja na propaganda. Uainishaji huu umefanywa kwa kigezo kimoja cha kazi kuu ya kihoja ili kuhakikisha kwamba mikakati iko katika kiwango kimoja cha uchanganuzi. Matokeo yanaonyesha kuwa mikakati hiyo huingiliana. Kujisawiri hujenga uaminifu wa msemaji; uwasawiri hasi huudhoofisha uaminifu wa mpinzani; uhalalishaji na uharamishaji hujadili chanzo na matumizi ya mamlaka; rufaa ya hisia hujenga mshikamano wa kihisia; na ubandikaji majina na propaganda huunda lebo na masimulizi yanayorahisisha hukumu ya kisiasa.

Kwa kuonyesha namna lugha inavyotumika kama rasilimali ya ubishi katika jukwaa lisilo rasmi la kiraia, utafiti huu unatimisha kuwa diskosi ya Nuru Okanga inaonyesha kwamba mamlaka ya kisiasa katika mawasiliano haijengwi na wadhifa rasmi pekee. Inaweza pia kudaiwa kupitia historia ya kibinafsi, uzoefu wa mashinani, uhusiano wa kiishara, utambulisho wa pamoja na madai ya uwajibikaji. Hata hivyo, matokeo haya hayawezi kutumiwa kuthibitisha athari halisi za diskosi kwa hadhira kwa sababu utafiti haukukusanya data ya mapokezi.

**Mapendekezo:** Tafiti zijazo zinaweza kuchunguza jinsi hadhira ya Bunge la Wananchi inavyopokea na kutafsiri mikakati hii, kulinganisha diskosi za Nuru Okanga na za wanaharakati wengine wa mashinani, na kuchunguza jinsi mikakati ya ubishi hubadilika wakati diskosi ya ana kwa ana inaposambazwa na kuzungushwa katika *YouTube*, *TikTok*, *Facebook* na X.

## MAREJELEO

Beard, A. (2000). *The language of politics*. Routledge.

Calleb Otieno, D., Kabala, N., Scott-Villiers, P., Gachihi, G., & Muthoni Ndung'u, D. (2016). Men and women of words: How words divide and connect the Bunge La Mwananchi Movement in Kenya. *IDS Bulletin*, *41*(1), 99–111. https://doi.org/10.19088/1968-2016.109

Charteris-Black, J. (2005). *Politicians and rhetoric: The persuasive power of metaphor*. Palgrave Macmillan. https://doi.org/10.1057/9780230501706

Chilton, P. (2004). *Analysing political discourse: Theory and practice*. Routledge.

Constitution of Kenya. (2010). *The Constitution of Kenya*. National Council for Law Reporting. https://www.kenyalaw.org

Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (4th ed.). Sage Publications.

DIF MEDIA. (2026, June 24). *Nuru Okanga loses it! Brutal response to Ruto's 'goons' order during June 25th demonstrations Diskosi ya 3* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=bRqRs7GZ-Dw

Dimbu, S., Kobia, J., & Kanyua, M. (2025). Mkakati wa uhalalishaji wa kimamlaka katika hotuba teule za marais wa Tanzania katika vikao vya pamoja vya mabunge ya kitaifa, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies, 8*(2). https://www.researchgate.net/publication/395309620

Fairclough, N. (2003). *Analysing discourse: Textual analysis for social research*. Routledge.

Habwe, J. H. (1999). *Discourse analysis of Swahili political speeches* [Unpublished master's thesis]. University of Nairobi. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/c88be7f9-7fe2-4d45-acce-2341264236b1

Kamuru, C. K., Wanyama, J. K., & M'Ngaruthi, T. K. (2025). Balagha katika hotuba za wagombea wawili wa urais kwenye makongamano ya wajumbe nchini Kenya, mwaka wa 2022. *East African Journal of Swahili Studies, 8*(1), 490–504. https://doi.org/10.37284/jammk.8.1.3230

Kariuki, T. N., & Gichanga, R. (2025). Social media coordination as a strategic messaging platform for political advocacy in Kenya: A case study of Kenya's gen Z uprising in 2024. *African Multidisciplinary Journal of Research*, 2(2), 100–124. https://doi.org/10.71064/spu.amjr.2.2.2025.430

Kenya Newsline. (2026, May 19). *Nuru Okanga goes crazy on fuel maandamano, Rachael death, burnt with petrol over Ruto photo on chest Diskosi ya 1* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=fd_kaZKttKI

Kenya Newsline. (2026a, February 10). *Nuru Okanga: Mumefanya Raila akakufa bila kua rais, 2027 ndio mtajua tulikua tunafuata Raila sio ODM Diskosi ya 5* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=shnQs2L4T60

Kenya Newsline. (2026b, June 23). *Nuru Okanga to Sifuna: Stupid! Wacha kusema sisi ndio Sifuna na wewe ni muoga unaenda kortini. Toka ODM* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=suuRMZHcFy0

Kenya Newsline. (2026c, June 26). *Wajaluo mumesoma lakini hamna akili. Adui mkubwa wa wajaluo ni Ruto! Nuru Okanga on WANTAM reality Diskosi ya 7* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=8CKEfyetELw

Khajavi, Y., & Rasti, A. (2020). A discourse analytic investigation into politicians' use of rhetorical and persuasive strategies: The case of US election speeches. *Cogent Arts & Humanities, 7*(1), Article 1740051. https://doi.org/10.1080/23311983.2020.1740051

Kiguta, G. M., Onyango, O. J., & Simwa, W. S. (2024). Uchanganuzi wa mikakati ya lugha katika diskosi ya kigaidi katika magazeti ya Kenya na ya kimataifa. *East African Journal of Swahili Studies, 7*(1), 463–476. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

Kimari, W., & Rasmussen, J. (2010). Public spaces and informal politics in Nairobi. *Journal of Eastern African Studies, 4*(3), 435–449. https://doi.org/10.1080/17531055.2010.487338

Kipkoech, G. (2022). Connections between internet, social media news use, and political participation in Kenya. *Social Science Computer Review*, 41(3), 871–885. https://doi.org/10.1177/08944393211058702

Kiplimo, C. E., Githinji, P., & Chacha, L. M. (2026). Dhima ya deksia katika kujenga mshikamano wa matini teule. *East African Journal of Swahili Studies, 9*(1), 88–105. https://doi.org/10.37284/jammk.9.1.4446

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International Publishers.

Lockwood, P. (2019). 'Before there is power, there is the country': Civic Nationalism and political mobilisation amongst Kenya's opposition coalitions, 2013–2018. *The Journal of Modern African Studies*, 57(4), 541–561. https://doi.org/10.1017/s0022278x19000491

Muigai, M. G. (2026). A discourse analysis of politicians' metaphoric utterances as reported in Kenyan newspapers. *Egerton Journal of Humanities, Social Sciences & Education, 14*(1), 13–26. https://eujournals.egerton.ac.ke/index.php/ejh/article/view/179

Mutembei TV. (2026, May 20). *Nuru Okanga is back on the MIC!! Kenyans watch him with their mouths wide open as he dispenses wisdom Diskosi ya 2* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=z5dXFN6Iyjg

Mutembei TV. (2026b, June 12). *"Western ni WANTAM!" Nuru Okanga launches fresh attack on Ruto at Jacaranda! Diskosi ya 4* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=tWppp4BhaZQ

Ohaga, O., & Emojong', O. (2024). Examining freedom of expression in Bunge La mwananchi forums in Kenya using the public sphere theory. *Online)* |, 4(2), 2790–1106. https://journals.jozacpublishers.com/index.php/jahca/article/download/777/411/2079

Shiracko Media. (2025, November 25). *Breaking! Am ready to die! Nuru Okanga faces president William Ruto on a live camera Diskosi ya 6* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=A39yGEWSNUM

van Dijk, T. A. (1998). *Ideology: A multidisciplinary approach*. Sage Publications.